

ASb
approved



Kiswahili


Ajali mbaya
Ursula Nafula
Rob Owen



Mimi na dadangu
tulikuwa
tukitembea kando
ya barabara.



Tuliona lori kubwa
likiendeshwa
kwenye mteremko.



Wakati huo, gari
ndogo liliendeshwa
kwa kasi kuelekea
upande wa juu wa
barabara.



Dereva wa lori
hakuwa
mwangalifu.

Alikuwa
akizungumza kwa
simu ya rununu.



Mara lori liligonga
gari!



Baadaye,
ambulansi ilifika
pamoja na polisi.



Pia magari mawili
ya kuvuta yale
yaliyohusika kwa
ajali yalifika.



Tulishuhudia kila
kitu.

Tulitishika sana.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Ajali mbaya

Author - Zanele Buthelezi, Thembani Dladla and Clare Verbeek

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© School of Education and Development (Ukzn) and African Storybook Initiative 2007

Creative Commons: Attribution 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.akdn.org

